



## **TAARIFA KWA WAANDISHI WA HABARI**

Sisi wananchi wa Kenya, tunaajumlisha Wakenya wa asli mbali mbali, na kuunganisha wahusika pamoja na taasisi mbalimbali, pamoja na vikundi vya wanawake, mashirika ya kiraia, vyama vya vijana, vikundi vya kitaaluma, viongozi wa dini, mashirika ya kijamii na taasisi za watu wenye ulemavu, tumekuja pamoja chini ya bendera ya “deCOALonize KENYA”, ili hukakikisha utekelezaji kamili wa haki zinazotolewa chini ya Ibara ya 42 ya Katiba ya Kenya ambayo inatoa kwamba: *"Kila mtu ana haki ya kuishi katika mazingira safi na salama"*. Kwa kufanya hivyo, tunapinga hatua ya serikali ya Kenya kukiuka katiba na kuanzisha mradi wa makaa ya mawe hapo Lamu na mradi wa madini ilopendekezwa Kitui.

Mbali na Katiba, mnamo mwaka wa 2016, Kenya ilinakili Mkataba wa Paris ulio ndani ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa (UNFCCC). Malengo ya Mkataba wa Paris, pamoja na mambo mengine ni kuongeza uwezo wa kukabiliana na athari mbaya za mabadiliko ya hali ya hewa na kuboresha ustahimilivu wa mabadiliko ya hali ya hewa na kupunguza gesi chafu. Kwa kuanzisha mmea wa makaa ya mawe ya Lamu na madini ya makaa Kitui, Kenya inapingana na Mkataba wa Paris na majukumu yake ya kimataifa kwa kuchangia uzalishaji wa gesi chafu.

Tangu mwaka wa 2001, Kamati ya Urithi wa Dunia imeandika mji wa Kae wa Lamu kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia ya UNESCO (UNESCO World Heritage List). Baada ya kujenga mradi wa makaa ya mawe karibu na rasilmali hii, bila ya shaka, visiwa vya Lamu viliyo na umuhimu mkubwa kihistoria vitaathirika. Mradi wa makaa ya mawe hauwezi kudumishwa na utaharibu vikubwa maliasili ambayo raia wengi wa Lamu wanategemea ikiwa ni pamoja na matumbawe na mimea ndani ya Visiwa vya Nyaraka. Wajumbe wa jamii ya Lamu wanategemea. Jamii wengi wa Lamu wanategemea kaszi zinazohusika na maliasli kama vile uvuvi, kilimo, kazi

ya mikoko na kadhalika, ambazo wataalam wamethibitisha zitaathirika vikubwa kutokana na ujenzi wa mradi wa makaa ya mawe.

Tikilinganisha na Afrika Kusini, miongoni mwa athari zinazotarajiwa ni kusababisha uzazi wa mapema katika Lamu inakadiriwa takriban 1,600 kwa mwaka. Madhara ya gesi ambayo yatatolewa na mradi huu yataenezwa mbali kuliko Lamu, kumaanisha kwamba Pwani yote, Garissa na pia Mtito Adei itaathirika.

Nao jamii ya Kitui inakabiliwa na kuhamishwa kutoka ardhi zao, kukabiliwa na hatari ya kuambukizwa na magonjwa ya kupumua, uchafuaji wa vifaa vya maji, uharibifu wa misitu, udongo, na mengi zaidi. Wilaya zote za Lamu na Kitui zitaathirika hata kama miradi itafungwa kwa sababu ya matatizo ya kudumu kama aside kutoka kwa mgodi, uchafuzi wa jivu unaoweza kuendelea kwa miaka mingi.

Kinachofanya mambo kuwa mabaya zaidi ni kwamba kwa sasa Kenya inayo umeme wa ziada ikilinganishwa na matumizi. Nchi yetu iko kati ya nchi saba duniani zinazoongoza kwa kuwa na rasilimali kubwa ya kioevu, na iliyo na nishati safi za kutosha. Zaidi ya hayo, kuna mwanga wa jua na upepo mwingi ambao unaweza kutumika kwa uwekezaji mdogo zaidi ili kuzalisha nishati endelevu zaidi. Yasikitisha kwamba wakati hali ya kimataifa kwa sasa nchi zinafunda miradi ya makaa ya mawe, lakini Kenya inaikumbatia ilihali ikiathiri mazingira na afya ya watu wake.

Tungependa pia kutangaza kuwa tunawaunga wenzetu mjini Lamu ambao hivi karibuni wamekamatwa na Idara ya Polisi kwa kufanya maandamano ya amani huko Lamu na wamekataliwa haki ya kukutana kwa amani inayopewa na katiba. Washirika wawili wa Save Lamu, Walid Ahmed na Ishaq Abubakar, wnagekuwa pamoja nasi leo lakini wajo mahakamani hivi leo Lamu kusikizwa kesi yao. Tunatoa wito ili kesi yao ifutwe na mashtaka yote yaondolewe ili haki yao ya kikatiba iimarishwe.

Kulingana na ahadi yetu na uthibitisho wa mazingira safi, sisi tunapinga mipango yote ya serikali na watendaji wengine wa kuanzisha mtambo wa makaa ya mawe katika Kaunti ya Lamu pamoja na uchimbaji wa madini Mui, Kaunti ya kitui na tuna orodhesha masharti yafuatayo:

1. Kuondolewa kwa haraka shughuli zote za ujenzi wa makaa ya mawe Katiba Kaunti ya Lamu.
2. Kuondolewa kwa haraka shughuli zote za madini ya makaa ya mawe katika Kaunti ya Kitui;
3. Kupitua sheria za kupeana leseni ya NEMA ili kuhusisha ushiriki wa umma bora zaidi ili kuzuia ukatili katika usimamizi wa mazingira nchini Kenya;
4. Kuwahambua viongozi wote wa umma ikiwa ni pamoja na Waziriambao walihusika katika kupitisha madini ya makaa ya mawe Kitui na mradi wa makaa ya mawe Lamu;
5. Mapitio ya sera ya nishati nchini Kenya kwa lengo la kupiga marufuku makaa ya mawe kabisa nchini Kenya.

Hakuna kitu kama “makaa ya mawe safi” (clean coal). Nishati ya makaa ya mawe ni chafu na sisi sote tunawakaribisha Wakenya kujiunga na harakati deCOALonize Kenya kupinga kila miradi ya makaa ya mawe nchini Kenya.

**Harakati ya deCOALonize**

**Siku ya Dunia ya Mazingira**

**5 JUNI 2018**